

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
*OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA*  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE**  
*(Mawasiliano yote yafanywekupitiakwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya)*

Simu Na.: 0262782111 Mkurugenzi

Fax Na. 0262782857

E-mail: [ded@njombedc.go.tz](mailto:ded@njombedc.go.tz)

[Info@njombedc.go.tz](mailto:Info@njombedc.go.tz)

Tovuti: [www.njombedc.go.tz](http://www.njombedc.go.tz)

*Unapojibu tafadhali taja:-*



S.L.P 547,  
NJOMBE

Kumb. Na. NDC/I.20/6/VOL.VII/135

06/11/2020

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe anawatangazia **nafasi 5** za kazi na anakaribisha maombi kwa watanzania wote wenye sifa na uwezo, kwa ajili ya kujaza nafasi za kazi kama zilivyo orodheshwa katika tangazo hili.

### 1. MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III – NGAZI YA MSHAHARA TGS B (NAFASI 4)

#### a) Sifa za mwombaji.

Mwenye elimu ya kidato cha nne au sita aliyehitimu mafunzo ya Astashahada /Cheti katika moja ya fani zifuatazo. Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambulika na Serikali.

#### b) Kazi na majukumu

- Afisa masuuli na mtendaji Mkuu wa Serikali za Kijiji
- Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa Utawala bora katika Kijiji.
- Katibu wa Mikutano na kamati za Halmashauri ya Kijiji.
- Kutafsiri na kusimamia sera, Sheria na taratibu.
- Kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umasikini na kuongeza uzalishaji mali.

- Kiongozi wa wakuu wa vitengo vya Kitaalam katika Kijiji.
- Kusimamia kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
- Mwenyekiti wa kikao cha wataamu waliopo katika Kijiji.
- Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi.
- Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Kijiji.
- Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

## 2. MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II – NGAZI YA MSHAHARA TGS B (NAFASI 1)

### c) Sifa za mwombaji.

Waombaji wawe wamehitimu kidato cha nne au cha sita wenye cheti cha utunzaji kumbukumbu katika mojawapo ya fani za afya masijala mahakama na ardhi.

### d) Kazi na majukumu

- Kutafuta kumbukumbu/nyaraka/mafaili yanoyohitajiwa na wasomaji.
- Kudhibitisha upokeaji, uandikishaji wa kumbukumbu/nyaraka
- Kuchambua kuorodhesha na kupanga kumbukumbu /nyaraka katika makundi kuringana na somo husika (classification and boxing) kwa ajili ya matumizi ya ofisi .
- Kuweka/kupanga kumbukumbu /nyaraka katika reki (file rakes/ cabinets) katika masijala / nyumba ya kuhifadhia kumbukumbu.
- Kuweka kumbukumbu (barua,nyaraka nk) katika mafaili .
- Kushughulikia maombi ya kumbukumbu /nyaraka kutoka taasisi za serikali.

## 3. MAELEKEZO

- Waombaji wote wawe raia wa Tanzania ambao hawazidi umri zaidi ya miaka 45 na hawapungui umri wa miaka 18.
- Waombaji wote lazima waambatanishe wasifu binafsi (CV) zenye wadhamini wawili na mawasiliano ya uhakika, anuani, barua pepe na namba za simu.

- iii. Waombaji wote waombe kwa kufuata masharti ya TANGAZO LA KAZI,
- iv. Waombaji lazima waambatanishe nakala za vyeti vifuatavyo:-
  - a) Astashahada/Cheti cha utaalumu kulingana na sifa za nafasi husika.
  - b) Cheti cha mtihani wa kidato cha nne au sita.
  - c) Cheti cha kuzaliwa.
  - d) Picha mbili za passport size.
- v. Hati ya matokeo ya kidato cha nne/sita (Result slip) na "Transcript" hazitafanyiwa kazi.
- vi. Watumishi wa Umma walioajiriwa wapitishe maombi yao kwa wajiri wao.
- vii. Waombaji wenye vyeti vya kidato cha nne na cheti cha taaluma ambavyo vimepatikana nje ya nchi wahakikishe vimehakikiwa na Baraza la mtihani la Taifa (NECTA) na Baraza la Elimu ya ufundi la Taifa (NACTE).
- viii. Barua ya maombi iandikwe kwa Kiswahili au kingereza.
- ix. Watakaoitwa kwenye usaili watajigharamia wenyewe.
- x. Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ni tarehe 19/11/2020 saa 9:30 alasiri, baada ya tarehe hiyo kupita maombi hayatapokelewa na watakao chaguliwa kufanya usaili watajulishwa tarehe ya usaili kupitia tovuti ya Halmashauri [www.njombedc.go.tz](http://www.njombedc.go.tz) na kwenye mbao za matangazo za Halmashauri.

Barua zote zitumwe kwa:-

MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE,  
S.L.P 547,  
**NJOMBE.**

Tangazo hili limetolewa na:-

  
Elitha J. Mligo  
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
**NJOMBE**